AckySHINE.com

# Kwa nini watu wanaamini kuwa Albino hawana maambukizo ya Virusi vya UKIMWI (VVU)?

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Imani hiyo si kweli kabisa. Inawezekana ni kupotoshwa kwa makusudi wa ukweli kuhusu jambo hilo kunakofanywa na watu wachache katika jamii ili kuendeleza matendo yao maovu. Watu wanaweza kufuata imani potofu na zisizo na msingi wowote ili kukwepa ukweli kuhusu VVU na UKIMWI. Kwa mfano; imani kuwa mtu anaweza kupona UKIMWI kwa kufanya mapenzi na bikira, mlemavu au Albino ni za uongo na hazina msingi wowote. VVU huambukizwa kupitia majimaji ya mwili, na njia kuu ya maambukizo ni kujamiiana bila kinga. Njia pekee za kuzuia maambukizo ni kuacha kabisa kufanya ngono, kuwa na mpenzi mmoja muaminifu au kutumia kondomu.Watu wanaoeneza imani hizi potofu wanatafuta njia mbadala ya kuhalalisha tabia zao mbaya.

Wewe pia kama Albino unatakiwa kupambana na imani hizo potofu kwani zinalenga kueneza madhara kwa watu wanaoishi na ualbino.